TANGAZO LA SERIKALI NA. 208 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA UDHIBITI NA USIMAMIZI WA MIFUGO YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 266 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama “Sheria Ndogo kuu”.

Marekebisho ya kanuni ya 5

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 5(h) kwa kuongeza maneno “na mifugo yao” mara baada ya neno “wengine”.

Marekebisho ya kanuni ya 11

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 11 kwa kufuta na kuiandika upya kanuni ndogo ya (3) kama ifuatavyo:

“(3) Halmashauri, ndani ya siku tatu kabla ya kuuza mfugo kwa mnada itamjulisha mmiliki na umma kuhusu kusudio hilo kwa njia ya matangazo ya maandishi au mdomo kadiri itakavyoonekana inafaa.”.

Dodoma,
10 Januari, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi – OR-TAMISEMI*